

## NOVENA KWA MTAKATIFU YUDA TADE(SIKU 9)

KUANZA TAREHE 19-27 OCTOBER 2021

Rozari ya Mt. Yuda Tade

Kwa jina la Baba.....

Penye medali ya Mt.Yuda Tade:

Mt.Yuda, Mtume mtukufu, Mtumishi amini na rafiki ya Yesu, jina la Yule mtoaji limewafanya wengi kukusahau. Walakini kanisa linakuhashimu na kukuomba kama msimamizi wa mashaka makubwa na wa mambo yasiyo na tumaini tena. Unionbee mimi mnyonge. Ninakuomba utumie uwezo ule uliojaliwa wa kuleta upesi msaada kwa watu walioukosa. Unisaidie sasa katika mahitaji yangu, ili nipate kitulizo na msaada wa uwinguni katika lazima zangu, masumbuko na mateso, hasa (*taja mahitaji yako*) pia ili niweze kumsifu Mungu nawe pamoja na wateule wote milele.

**ROZARI YA MT.YUDA TADE INA SHANGA TISA TU.KAMA KTK PICHA HAPO CHINI.**



Penye kila shanga tatu Sali: Salaamu Maria.....mara tatu

Kati ya seti ya shanga tatu na mkufu sali:

Mtakatifu Yuda, Mtume na Shahidi na jamaa wa bwana wetu Yesu Kristu, wa mbarikiwa Bikira Maria na Mtakatifu Yosefu, unionbee.

Sala ya Mwisho wa Rozari

Ee Mtakatifu Yuda, Mtume na shahidi, uliye mkuu katika fadhila na tajiri wa miujiza, jamaa wa karibu wa Yesu Kristu, mwombezi msaada mwaminifu wa wale wote waombao msaada wako nyakati za shida. Ninakukimbilia wewe na kusihi unisaidie, katika shida yangu hii (*Taja ombi lako*) Nami ninaahidi kukufanya ili ujulikane na watu wakuombe. Amina

Kwa jina la Baba.....

*Rozari hii ikiwa itasaliwa kwa imani thabiti kwa siku 9 mfululizo, haijawahi kushindwa.*

**Kutafsiriwa na Fortunata Masaka-Rozari Hai Mtandaoni. Avee Maria!**